

HALMASHAURI YA WILIYA YA MBEYA



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

16/03/2022


Halmashauri ya wilaya ya Mbeya inawatangazia wananchi, wafanya biashara, makampuni na taasisi mbalimbali mnada wa hadhara. Kwa idhini iliyotolewa na Katibu Mkuu Hazina halmashauri itauza kwa mnada wa hadhara MAGARI matano (5) na PIKIPIKI tisa (9) siku ya tarehe **5/04/2022** hadharani **kuanzia saa 4:00 asubuhi**. Mnada utafanyika kwenye karakana ya halmashauri iliyoko nyuma ya ofisi za Ardhi za halmashauri ya jiji la Mbeya.

MALI ZITAKAZOUZWA NI KAMA IFUATAVYO:

1. NISSAN PATROL MOJA(1)
2. TOYOTA LAND CRUISER HARD TOP MOJA(1)
3. TOYOTA LAND CRUISER GX MOJA(1)
4. LAND ROVER 110 MOJA(1)
5. ISUZU TX MOJA (1)
6. PIKIPIKI TISA(9)

MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi anatakiwa kulipa 25% ya bei ya mnada na kiasi kilichobaki kitalipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2. Ukaguzi wa mali husika utafanyika siku moja kabla ya siku ya mnada kuanzia 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
3. Gharama za kubadilisha umiliki (**transfer of ownership**), kodi na gharama nyingine zote ni jukumu la mnunuzi.
4. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
5. Mnunuzi atawajibika kuondoa /kuchukua mali aliyonunua ndani ya siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
6. Malipo yote yatalipwa kupitia mfumo wa malipo ya serikali.


Stephen E. Katemba
Mkurugenzi mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya Mbeya